



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
WAKATI WA KUWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16**

Mhe. Samia Suluhu Hassan (Mb.),

Waziri wa Nchi, Muungano

Mhe. Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb.),

Waziri wa Nchi, Mazingira

Dodoma

Mei, 2015

YALIYOMO

I. UTANGULIZI.....	1
II. MASUALA YA MUUNGANO.....	4
III. HIFADHI ENDELEVU YA MAZINGIRA.....	13
IV. MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU39	
VI. SHUKRANI NA HITIMISHO.....	42
VII. MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/16.....	43

DIRA

'Tanzania yenye Muungano imara na Mazingira safi, salama na endelevu'.

DHIMA

'Kuwa na ufanisi katika kuimarisha Muungano na kuongeza ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano, na kuratibu usimamizi wa Mazingira ili kuboresha ustawi wa watanzania'

MAJUKUMU YA OFISI

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la Majukumu ya Wizara la mwezi Desemba, 2010, (*Assignment of Ministerial Responsibilities Government Notice No.494 of 17th December, 2010*), majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais yameainishwa kama ifuatavyo:-

- i) Kuratibu masuala ya Muungano;
- ii) Kuratibu ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yasiyo ya Muungano; Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira;
- iii) Kusimamia na kuendeleza watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais;
- iv) Kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji wa Idara zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais; na Kusimamia shughuli za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

I. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2014/15; na malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2015/16.
2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote napenda kuwashukuru kwa dhati, Waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa **Jason Samson Rweikiza (Mb.)**, na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa **James Daudi Lembeli (Mb.)** kwa kupokea na kuchambua taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/15, na pia kujadili na kupidisha malengo na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2015/16. Vilevile, natoa shukrani kwa Wasemaji Wakuu wa Kambi ya Upinzani, Mhe. Mchungaji **Israel Natse (Mb.) (Mazingira)** na Mheshimiwa **Tundu Antiphas Lissu (Mb.) (Muungano)** kwa ushirikiano wao wa dhati na michango yao katika kuboresha hoja hii ninayoiwasilisha leo hapa bungeni.
3. *Mheshimiwa Spika*, kabla ya kuwasilisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii ya kipekee kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mafanikio

makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini katika Awamu ya Nne ya utawala wa Serikali. Mafanikio yaliyopatikana ni matokeo ya uwezo na umakini wake katika uongozi. Ni ukweli ulio dhahiri kuwa, nchi yetu imepata mafanikio ya kiuchumi na kijamii katika kipindi chake cha uongozi. Tanzania imezidi kutambulika kimataifa hasa katika kuchangia juhudzi za kuleta amani katika Bara la Afrika na kusimamia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi wa Afrika ya Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, napenda kutumia nafasi hii, mimi binafsi na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Mazingira na Naibu Waziri – Ofisi ya Makamu wa Rais, kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupa dhamana ya kuratibu masuala ya Muungano na hifadhi ya Mazingira nchini katika kipindi cha uongozi wake.

4. *Mheshimiwa Spika*, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. Mohammed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini na wa hekima ambao umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika masuala ya Muungano na usimamizi wa hifadhi ya Mazingira nchini.
5. *Mheshimiwa Spika*, napenda pia kutoa pongezi za dhati kwa Bunge lako tukufu kwa kazi nzuri ambayo limeifanya kwa kipindi chote cha uongozi wako. Nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza Bunge letu tukufu kwa busara ya hali ya juu katika kutimiza majukumu yake na wajibu kwa wananchi wa Tanzania. Nakupongeza pia kwa kuliwakilisha vizuri Bunge na nchi yetu katika Mabunge ya jumuiya mbalimbali, hususan kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Bunge la SADC. Tunakuombea kila la kheri na mafanikio katika majukumu makubwa uliyonayo.

6. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii sasa kuwapongeza Mheshimiwa **Dkt. Grace Pujah (Mb)** na Mheshimiwa **Dkt. Innocent Seba (Mb)** kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatachia utekelezaji mzuri wa majukumu yao mapya ya kuwatumikia wananchi wa Tanzania.
7. *Mheshimiwa Spika*, nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa tathmini ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15 na malengo na mwelekeo kwa mwaka wa fedha 2015/16. Aidha, niwatakie Mawaziri wote watakaofuata kila jema na ufanisi katika kazi hii inayotukabili.
8. *Mheshimiwa Spika*, kwa masikitiko makubwa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa ndugu, marafiki na wananchi, kwa kifo cha Mheshimiwa **Kapt. John Damiano Komba**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi, kilichotokea mwezi Februari, 2015. Aidha, natoa pole za dhati kwa wananchi kwa ujumla, kwa kuwapoteza ndugu zao na mali kutokana na matukio ya ajali za barabarani na maafa ya mafuriko na mvua kubwa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Vifo na majanga yaliyotufika ni pigo kubwa kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu. Tutawakumbuka kwa juhudhi zao, na tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.
9. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kusema hayo, napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, pamoja na malengo kwa mwaka wa fedha 2015/16.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15, UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2015/16

10. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu iliyokabidhiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2010 – 2015); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2010 - 2015; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II); Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997; na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004.

11. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi ya Makamu wa Rais iliweza kutekeleza kazi zilizokuwa zimelengwa katika uratibu wa masuala ya Muungano na ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano; na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya usimamizi wa Mazingira hapa nchini. Utekelezaji ulifanyika kulingana na upatikanaji wa fedha.

II. MASUALA YA MUUNGANO

12. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi kuititia hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/15 iliahidi mambo kadhaa, ambayo utekelezaji wake umeendana na maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 kama yalivyo kwenye Ibara ya **184**. Uhalsia wa utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Kuondoa vikwazo katika utekelezaji wa masuala ya Muungano

13. *Mheshimiwa Spika*, jitihada za Ofisi za kuondoa vikwazo katika utekelezaji

wa mambo ya Muungano ziliendelezwa kwa kufuatilia utatuzi wa masuala ya Mahusiano ya Kifedha baina ya SMT na SMZ. Masuala hayo ni pamoja na: hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki; mgawanyo wa faida ya Benki Kuu; malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili; uchimbaji wa mafuta na gesi asili; na usajili wa vyombo vya moto.

14. *Mheshimiwa Spika*, sekta za fedha za SMT na SMZ baada ya kuangalia mawasiliano yaliyofanywa baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iliyokuwa Bodi ya sarafu ya Afrika Mashariki, kwa pamoja, zimekubaliana kuwashirikisha Wanasheria Wakuu wa SMT na SMZ watoe ushauri wa kisheria kabla ya Waraka uliotayarishwa kupelekwa kwenye kikao cha pamoja cha SMT na SMZ.

15. *Mheshimiwa Spika*, sekta za fedha zinaendelea kujadiliana kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili kwa kuangalia vipengee na masharti yatakayofanya SMZ na SMT kukubaliana kutumia mfumo mpya wa malipo, kwa walipa kodi waliopo Zanzibar, jambo ambalo litasaidia kuondoa manung'uniko kwa wafanyabiashara.

16. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na kwamba suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia limekubalika kuondolewa katika mambo ya Muungano, bado SMT na SMZ zinaendelea na mawasiliano ya jinsi kazi ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi itakavyofanywa kwa kuzingatia sheria za hapa nchini na zile za kimataifa.

17. *Mheshimiwa Spika*, fursa iliyotokea ya kutunga Katiba Mpya ya nchi yetu imetoa wasaa mzuri wa kuyapa hadhi ya kikatiba masuala mengi ya Muungano ambayo Serikali zetu za SMT na SMZ zilikubaliana na

mustakabali wa uendeshwaji wake. Baadhi ya mambo hayo ni; suala la ushirikiano na uhusiano wa Zanzibar na Taasisi za Kikanda na Kimataifa kwa mambo yanayohusu Zanzibar, Ibara ya **76**; uwezo wa SMZ kukopa fedha ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (Ibara ya 261) ambapo utaratibu huu utarahisisha upatikanaji wa mikopo kwa maendeleo na ustawi wa Zanzibar. Suala jengine ni ajira kwa wananchi wa pande zote mbili katika taasisi za Muungano, ambapo Tume ya Uhusiano na Uratibu wa mambo ya Muungano imepewa jukumu la kusimamia uwepo wa uwakilishi wa pande zote mbili za Muungano, (Ibara 128 (1) (f) na 128 (3), na kutiliwa mkazo katika Ibara 150 (4) iliyoweka wazi uzingatiaji wa uwakilishi wa pande mbili za Muungano kwa nafasi za uteuzi.

- 18. *Mheshimiwa Spika*, ni matumaini yetu kwamba, mchakato huu utakapokamilika, na kama Katiba inayopendekezwa itakubaliwa na wananchi, changamoto nyingi za Muungano zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi.**

Uratibu wa Masuala ya Kiuchumi, Kijamii na Kisheria na Mambo Yanayohusiana na Katiba katika Muungano kwa faida ya pande mbili za Muungano

- 19. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Makamo wa Rais ikiwa ndie Mratibu Mkuu wa masuala ya kiuchumi na kijamii yanayotekelizwa ki-muungano, imeratibu gawio la fedha la asilimia 4.5 kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kusaidia kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Gawio hilo hujumuisha misaada ya kibajeti, fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania na Kodi ya Mishahara (PAYE) kwa wafanyakazi wa taasisi za Muungano. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, SMZ ilipokea shilingi **27,681,808,403/=** kati ya shilingi **44,039,608,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo shilingi **7,137,882,543/=** ni**

gawio la kibajeti kwa SMZ, shilingi **15,750,000,000/=** ni fedha za Kodi ya Mishahara, shilingi **1,243,925,860/=** ni fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na shilingi **3,200,000,000/=** ni gawio la faida ya Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, SMZ imepokea shilingi **350,000,000/=** ikiwa ni deni la fedha zilizotumiwa na SMZ wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya miaka **50** ya Muungano.

20. *Mheshimiwa Spika*, miradi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi kiuchumi na kijamii imeendelea kuibuliwa. Utekelezaji wa miradi inayolenga kuboresha elimu, afya, masoko, maji, mazingira pamoja na usafiri na usafirishaji unaimarishwa ili kujenga jamii ya watanzania wenyewe uwezo wa kupambana na umaskini. Baadhi ya miradi ambayo hufadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na wahisani wa maendeleo ni pamoja na utekelezaji wa malengo ya kazi za TASAF III yanayoendelea kufanyika kwa mafanikio katika pande zote mbili za Muungano. Mpango wa kunusuru Kaya Maskini umetekelizwa kwa kaya zipatazo **1,000,000** za Halmashauri **159** za Tanzania Bara na Wilaya zote za Tanzania Zanzibar. Mpango huu unafaidisha watu wapatao milioni **7** ambao ni karibu asilimia **15** ya Watanzania wote. Malipo yaliyofanyika kwa kaya za walengwa ni shilingi **41,989,439,745/=** kwa upande wa Tanzania Bara na shilingi **240,205,767/=** kwa Zanzibar. Fedha hizo zinatumika katika kuboresha maisha ya watoto katika kaya zilizofaidika kwa kupatiwa lishe bora, elimu na afya, na pia kutoa fursa za ajira za muda. Aidha, Mpango huu una malengo ya kuinua hali ya maisha kupitia uwekaji wa akiba na kuwekeza kwenye shughuli za kiuchumi.

21. *Mheshimiwa Spika*, miradi mengine ni ile ya programu ya kuimarisha Huduma za Kilimo na kuendeleza Sekta ya Mifugo (ASDPL/ ASSP) Miradi hii imestawisha hali za maisha ya wakulima na wafugaji walio chini ya mradi

huu, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wenye tija, kipato na uhakika wa chakula. Kwa mwaka huu wa fedha, Programu hii imekamilika na Serikali iko katika hatua za maandalizi ya awamu ya pili ya programu.

22. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa Awamu ya pili ya Programu inayoendeshwa na Mfuko wa Changamoto za Milenia (MCA-T) umepangwa kutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, kwenye miradi ya Sekta za Nishati. Programu inalenga kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kukarabati mfumo wa umeme katika mji mkongwe Zanzibar na katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania Bara; kujenga uwezo wa kitaasisi kwa TANESCO na ZECO; na kukuza Sekta ya nishati kwa kushirikisha sekta binafsi kwa Zanzibar pekee.
23. *Mheshimiwa Spika*, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unatekeleza kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara zoezi la upimaji wa ardhi limezalisha viwanja **8,091** katika Halmashauri za Njombe, Babati, na Tunduma, pamoja na Manispaa za Iringa, Morogoro, Kinondoni na Arusha. Kwa upande wa Zanzibar, upimaji umefanywa kwenye shehia za Limbani, Jang'ombe na Welezo, ambapo viwanja **4,130** vilipimwa, na Vijiji vya Kiungoni, Chwaka, Chokocho na Nungwi vilipimwa na viwanja **4,307** vimepatikana. Mpango huu unaendelea na zoezi la uratibu wa kutoa hati za kimila kwa wamiliki wa mashamba pamoja na urasimishaji wa biashara katika baadhi ya Halmashauri.
24. *Mheshimiwa Spika*, Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini – (MIVARF) yenye dola za Marekani milioni **169.5** unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa

kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Taasisi ya Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA). Lengo la Mpango huu ni kupunguza umaskini na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi endelevu, kwa kuziwezesha kaya maskini za vijijini, katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuongeza kipato na usalama wa chakula.

25. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2014/15 kazi zilizoteklezwa chini ya programu hii ni pamoja na: ukarabati wa kilomita **369** za barabara, kati ya kilomita **555.3** zilizopangwa katika Halmashauri **18** za Tanzania Bara na Zanzibar; ujenzi wa masoko na maghala manne **(4)** na matatu **(3)** yamekarabatiwa; vikundi vyta wajasiriamali **102** vyta Zanzibar, na **294** vyta Tanzania Bara vimeunganishwa na masoko; kuwezesha benki za wananchi (Community Banks) kupanua wigo wa huduma kwa jamii maskini za vijijini; na kukuza ufanisi kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo.

26. *Mheshimiwa Spika*, ili taasisi za Muungano ziweze kufanyakazi kwa ufanisi na kusogeza huduma kwa wananchi, jitihada za kujenga au kuanzisha Ofisi za kudumu kwa upande wa Zanzibar ziliendelea. Mwaka wa fedha 2014/15, Idara ya Uhamiaji imemaliza ujenzi wa jengo la Makao Makuu Zanzibar, na kulizindua rasmi tarehe 25 Aprili, 2015. Aidha, Mamlaka ya Vitambulisho vyta Taifa (NIDA) imewekwa katika jengo la zamani la uhamiaji na imefungua matawi yake katika wilaya zote za Zanzibar. Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Kamisheni ya Nguvu za Atomiki (TAEC) zimepata Ofisi za Kudumu huko Maruhubi Zanzibar, na taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la taasisi hiyo huko Buyu Zanzibar.

Kuelimisha Umma kuhusu Muungano

27. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano kupitia majarida, vipeperushi, na fulana zenyenye ujumbe wa Muungano zilizogawiwa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Zanzibar, Iringa, Mbeya na Dodoma. Aidha, Ofisi inakamilisha toleo la pili la Kitabu cha taarifa ya mafanikio ya miaka **50** ya Muungano, sanjari na kukamilishwa kwa kitabu cha mafanikio ya masuala ya Muungano katika Awamu ya Nne, kwa ajili ya kuelimisha umma. Pamoja na hayo, semina za elimu ya Muungano kwa wananchi zilifanywa huko Zanzibar. Ofisi kwa kushirikiana na Makumbusho ya Taifa imetoea elimu ya Muungano kwa wanafunzi **1500** wa shule za msingi za Mkoa wa Dar es Salaam, na kuandaa onesho la Muungano wakati wa maadhisho ya miaka **51** ya Muungano pamoja na kutoa elimu kwa watumishi **80** (Maafisa Viungo) wa Wizara na Taasisi za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano

28. *Mheshimiwa Spika*, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeratibiwa. Katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, wizara na taasisi zisizo za Muungano za SMT na SMZ hushirikiana katika kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya sera, utaalamu na wataalamu, ushiriki katika masuala ya kitaifa, kikanda na kimataifa, utafiti na ziara za mafunzo.

29. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka huu wa fedha, vikao vitano (5) vya ushirikiano vimefanyika katika sekta zinazosimamia masuala ya Tawala za

Mikoa na Serikali za Mitaa; utumishi katika Jamhuri ya Muungano; Uchukuzi; Biashara, na masuala ya utawala bora. Masuala yaliyojadiliwa katika sekta hizo ni pamoja na changamoto na mikakati ya ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; uwiano wa fedha zinazolipwa na wananchi na huduma zinazotolewa; uzoefu katika kuzuia na kupambana na rushwa; na maadili ya viongozi wa umma.

- 30. *Mheshimiwa Spika*,** masuala mengine yaliyojadiliwa yanahusu nafasi za ajira katika Taasisi za Muungano; kufungua Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Zanzibar; na mikakati ya kudhibiti bidhaa zisizo na viwango, na bandari zisizo rasmi ambazo zimekuwa mwanya wa kuitisha biashara na wahamiaji haramu, majahazi yasiyosajiliwa na vitendo vingine viovu.

MALENGO YA MWAKA 2015/2016

- 31. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kitaifa, ikiwa ni pamoja na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi. Ofisi inalenga kwenye kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Muungano, na kudumisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa manufaa ya Watanzania wote.

- 32. *Mheshimiwa Spika*,** katika kulitekeleza hilo, Ofisi itaandaa na kuitisha kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kutafakari njia muafaka za kushughulikia masuala ya Muungano. Kikao hicho kitatanguliwa na kikao cha Mawaziri wa SMT na SMZ, kikao cha Makatibu Wakuu wa SMT na

SMZ na vikao vine (4) vya Sekretarieti ya SMT na SMZ.

33. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua nyengine ya kudumisha Muungano wetu, Ofisi itaendelea kuelimisha umma kuhusu Muungano kupitia redio, luninga, magazeti, majarida, vipeperushi, semina na maonesho ya kitaifa; kuongeza ufanisi katika uratibu wa utekelezaji wa miradi ya jamii inayolenga kuinua kipato kwa kaya masikini Mijini na Vijiji kwa lengo la kuziinua kiuchumi; na kushajiisha wizara au taasisi zisizo za Muungano zenyet kazi zinazoshabihiana SMT na SMZ kuendeleza mashirikiano kwa nia ya kukuza ustawi wa Watanzania.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2005 HADI 2015

34. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2015 Serikali imekuwa na mafanikio katika utekelezaji wa masuala ya Muungano. Mafanikio hayo ni pamoja na kukua kwa demokrasia nchini; kuimarika kwa ulinzi na usalama; amani na mshikamano; na uhuru wa kuabudu na kuishi popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni kuundwa kwa Kamati ya Pamoja SMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano. Kamati hii imeshughulikia hoja 15 za Muungano ambapo hoja 11 zimefanyiwa kazi kwa mafanikio na kutatua changamoto za Muungano.

35. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Awamu ya Nne ya Serikali, ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano umeimarika baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na hivyo kuimarisha na kuendeleza uhusiano baina ya wananchi wa pande mbili za Muungano.

36. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, ujenzi wa Ofisi na makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Tunguu Zanzibar na jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Mtaa wa Luthuli Dar es Salaam umefanyika. Makao Makuu ya Mamlaka ya Uvubi wa Bahari Kuu yamejengwa Zanzibar, Awamu ya kwanza ya Jengo la Sayansi ya Bahari huko Buyu, Zanzibar imekamilika, pamoja na majengo yaliyoainishwa katika Ibara ya **26** ya Kitabu hiki.

37. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza masuala ya Muungano, zipo changamoto zilizojitokeza ambazo ni: utatuzi wa hoja za Muungano kwa pande mbili zenye mifumo tofauti ya sheria; suala la uelewa wa jamii kuhusu masuala ya Muungano; na ufinyu wa bajeti.

III. HIFADHI ENDELEVU YA MAZINGIRA

MAELEKEZO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015 NA UTEKELEZAJI WAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15

38. *Mheshimiwa Spika*, Ibara ya **194** ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2010 – 2015, inaelekeza Serikali kutekeleza masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 hali halisi ya utekelezaji wa Ilani hiyo ni kama ifuatavyo:-

“Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti pamoja na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa vitongoji, mitaa, vijiji na kata watakiwe kuikagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati za vijiji, vituo vya afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa”.

39. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza maelekezo haya, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006 kwa kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Upandaji Miti milioni **1.5** kwa mwaka, kwa kila Halmashauri ya Wilaya. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imepokea taarifa za Mikoa **22** kuhusu miti iliyopandwa na kumea kwa mwaka wa fedha 2013/14. Taarifa hizo zinaonesha kuwa miti **217,301,650** ilipandwa na kati ya hiyo miti **181,720,849** imestawi, sawa na asilimia **83.63** ya miti iliyopandwa. **Kiambatisho Na.1** ni taarifa za upandaji miti kitaifa kwa mwaka 2013/14.

40. *Mheshimiwa Spika*, Halmashauri zilizopanda miti na kustawi kwa zaidi ya asilimia **80** ni **39** ambazo ni **Wilaya za Mbanga, Ilaje, Kyela, Mbeya Vijijini, Siha, Iringa, Kilwa, Ruangwa, Butiama, Musoma, Rorya, Ludewa, Njombe, Makete, Makambako, Wanging`ombe, Uyui, Ulanga, Gairo, Kilombero, Msalala, Kishapu, Shinyanga Vijijini, Shinyanga Mjini, na Maswa, Misungwi, Ukerewe, Mwanza jiji, Illemela, Newala, Nanyumbu, Mtwara vijijini, Manispaa ya Sumbawanga, Arusha, Meru, Longido, Monduli, Karatu na Kilindi.** Mikoa ambayo Halmashauri zake hazijawasilisha taarifa za upandaji miti kwa mwaka 2013/14 ni: Manyara, Kagera na Geita. Naipongeza Mikoa ambayo wilaya zake zimevuka lengo la upandaji miti, nahimiza mikoa mingine kuongeza juhudhi ili kulinda mazingira ya nchi yetu.

41. *Mheshimiwa Spika*, mashindano ya Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti yameendelea kuhamasishwa nchini katika ngazi za Kaya, Vijiji, Kata, Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa na Mikoa. Makundi mengine ni shule za msingi na sekondari; Vyuo vya

Mafunzo/Utafiti; Taasisi za Kijeshi; na Taasisi/Vikundi vyatuhamasishaji, uwekezaji na uvezeshaji. Utoaji wa tuzo hii umeimarisha upandaji wa miti nchini. Tuzo hii hutolewa kila baada ya miaka miwili (2) na itatolewa tena mwaka 2016 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, kitaifa. Orodha ya washindi na aina ya Tuzo walizopata zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2** cha Kitabu hiki.

“Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za hifadhi ya misitu”

42. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi iliendelea kuhimiza Wilaya na Manispaa kutunga sheria ndogo za hifadhi ya misitu, tathmini ya mazingira na usafi wa mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Halmashauri za Njombe, Kalambo, Mpanda, Uvinza, Kasulu, Kibondo, Kishapu, na Sengerema zilitunga sheria ndogo za kusimamia utunzaji wa Mazingira katika maeneo yao.

“Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe”

43. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kuhamasisha na kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi ya Mwaka 2004, Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa nchini.

44. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi kuitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kuratibu na kutekeleza Mkakati wa Usimamizi wa Mazingira ya Pwani kwa kukamilisha taarifa ya tathmini ya Matumbawe ambayo itasaidia kuweka mikakati ya kuhifadhi maeneo yanayohitaji uangalizi zaidi. Aidha, Baraza limeanza utekelezaji wa mpango wa dharura

wa kukabiliana na uchafuzi wa mazingira baharini (Marine Contingency Plan), kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), unaofadhiliwa na Serikali ya Norway.

45. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi na Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Kuridhiwa kwa marekebisho ya Mkataba na Itifaki yake yatachangia katika jithada za miradi hii ya kuhakikisha kuwa uchafuzi wa fukwe za nchi yetu unapungua.

“Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa Mazingira”

46. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara za Nishati na Madini, Maliasili na Utalii, Kilimo na Mifugo, pamoja na Tume ya Mipango, inaandaa mpango wa kuongeza matumizi ya nishati mbadala, mfano gesi asilia, ili kupunguza matumizi ya mkaa wa miti katika miji mikubwa, kwa kuanza na jiji la Dar-es-Salaam. Maandalizi ya mpango huu ni sehemu ya juhudhi za Ofisi za kupunguza uharibifu wa mazingira na kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kukamilisha Sera ya Uendelezaji wa Nishati nchini ili kuhakikisha matumizi ya nishati mbadala yanaenda sanjari na sera na mipango ya taifa ya kujilettea maendeleo endelevu. Katika mwaka 2015/16, Ofisi itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 itakayosisitiza matumizi ya nishati mbadala ili kuhifadhi mazingira. Aidha, baada ya mapitio ya Sera, Ofisi itaendelea na kuitia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

“Serikali kupunguza gharama za vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti”

47. Mheshimiwa Spika, kama nilivyolarifu bunge lako tukufu mwaka jana, Serikali imeendelea kusimamia uamuzi wa kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani, kwa asilimia **18** katika vifaa vya gesi na umeme, ili wananchi waweze kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kunusuru mazingira yetu. Aidha, gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijijini zimeendelea kubaki shilingi **27,000/=** tu na hivyo kuwafanya watu wengi zaidi vijijini kuunganisha umeme. Aidha, washirika wa Maendeleo, yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wameendelea kuchangia jitihada za Serikali kwa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala, mfano: nishati itokanayo na kinyesi cha mifugo (biogas) na umeme nuru (solar energy).

“Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara ili kutochafua mazingira”

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira iliendelea kufanya ukaguzi wa viwanda, biashara na migodi ili shughuli hizo zisichafue mazingira na kuhimiza uzingatiaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na ufuatiliaji wake. Jumla ya viwanda **15** vilifanyiwa ukaguzi wa Mazingira. Viwanda hivyo ni: MM Integrated Steel Mills Ltd; BIDCO Oil & Soap Ltd; Murzah Oil Mills Ltd; Auto Mech Limited; OK Plastic Limited; Basic Elements Ltd; na Twiga Cement vya Dar es Salaam. Viwanda vingine ni: Azam Fruit and Juices Industry; na Rhino Cement mkoani Pwani; Tanga Cement; Nilecanth Ltd; na Afritex Ltd; na PPPL mkoani Tanga; 21st Century Textile Mills, Morogoro; na Sunflag Textile Mill – Arusha.

49. *Mheshimiwa Spika*, katika zoezi hilo la ukaguzi, amri za katazo (Environmental Protection Orders) zilitolewa kwa viwanda vinne (4); amri za kusitisha shughuli (Stop Orders) zilitolewa kwa viwanda vitatu (3); na viwanda vingine vilipewa onyo na kutozwa faini kwa uchafuzi wa mazingira. Aidha, Baraza lilikagua eneo la Vingunguti ambako viwanda vilikuwa vinatiririsha majitaka kwenye Mto Msimbazi. Ukaguzi ulifanyika pia katika eneo la dampo la Pugu Kinyamwezi na maelekezo yalitolewa ya hatua za kuchukua.

50. *Mheshimiwa Spika*, viwanda na maeneo mengine yaliyofanyiwa ukaguzi wa mazingira na kupewa onyo ni pamoja na: Kiwanda cha Royal Soap and Detergents na Carmel Concrete Plant vilivyopo eneo la viwanda la Mabibo; Mwambao wa fukwe za Kunduchi kuhusu ukongoaji wa meli chakavu; shughuli za gereji katika makazi, eneo la Tabata Kinyerezi – Manispaa ya Ilala; na maeneo ya uchimbaji mchanga holela Bunju, Kigamboni – Gezaulole na Ubungo nyuma ya majengo ya Shirika la Viwango Tanzania. Amri za kusitisha shughuli za uchimbaji katika maeneo hayo zilitolewa.

51. *Mheshimiwa Spika*, ukaguzi wa mazingira ulifanyika pia katika eneo la ujenzi wa mtambo wa kusafisha majitaka wa Mnazi Bay mkoani Mtwara. Baraza lilibaini kasoro na kutoa amri ya kusitisha ujenzi wa bomba la kutiririsha majitaka kutoka kwenye mtambo kwenda baharini. Aidha, TPDC walielekezwa eneo ambalo majitaka yanaweza kumwagwa bila kuathiri viumbi bahari.

“Kutekeleza Mradi wa Vijiji vya Mfano vya Hifadhi ya Mazingira (Eco-Villages)”

52. *Mheshimiwa Spika*, kama nilivyolitaarifu Bunge lako tukufu mwaka jana,

awamu ya pili ya Mradi wa Vijiji vya Mfano (Eco-villages) unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, ulianza kutekelezwa mwaka 2013/14 katika Kanda za Maeneo ya Pwani na Ukanda wa Chini; Maeneo ya Miinuko yenyе mvua nyingi kiasi; na Maeneo ya Kanda Kame kwa gharama ya takriban shilingi bilioni **16**. Miradi hii ni muhimu katika kuonyesha mbinu zilizo bora za kuhahikisha shughuli za wananchi za kiuchumi na kijamii haziathiriwi na mabadiliko ya tabianchi. Taasisi tano (5) zinashiriki katika utekelezaji wa miradi mitano (5). Taasisi hizo ni: Community Forest Pemba (CFP) inayotekeleza Mradi Kisiwani Pemba kwa gharama ya EURO **1,250,000**; Heifer Nederland katika Wilaya ya Igunga kwa gharama ya EURO **2,132,480**; ONGAWA – Ingeniería para el katika Milima ya Usambara Mashariki kwa gharama ya EURO **1,364,449**; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - Dodoma kwa gharama ya EURO **1,999,802**; na Instituto Oikos Onlus Associazione katika Wilaya ya Arumeru kwa gharama ya EURO **1,796,262.50**. Miradi hii inatarajiwа kutekelezwa kwa kipindi cha miezi **48** hadi **54** kuanzia mwaka 2014.

“Kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira Katika Miradi ya Maendeleo”

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya miradi **870** ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Kati ya Miradi hiyo, 596 ni miradi ya sekta mbalimbali na **274** ni minara ya mawasiliano. Katika kipindi hiki, miradi **640** ilipatiwa Hati ya TAM (Environmental Impact Assessment - EIA Certificates). Baraza lilifuatilia miradi **121** katika mikoa ya Mbeya, Katavi na Morogoro, ambapo miradi **42** ni migodi, **13** ni viwanda, **56** ni vituo vya mafuta, hoteli mbili (**2**), mashamba matatu (**3**) na mingine minane (**8**) ya barabara, hospitali na duka la vipuri.

54. Mheshimiwa Spika, Baraza lilipokea maombi ya wataalamu binafsi **229** na

makampuni **38** ili kusajiliwa kufanya TAM na Ukaguzi wa Mazingira, baada ya uhakiki, wataalamu binafsi **108** na makampuni **25** yamesajiliwa. Napenda kutumia fursa hii kuwasihhi wataalam wote wa Mazingira nchini kuzingatia ipasavyo maadili ya kazi yao na maelekezo ya sheria, ili kwa pamoja tuweze kutunza mazingira yetu. Vile vile, maofisa wa Mazingira **35** walipatiwa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15 NA MALENGO YA MWAKA 2015/16

55. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, sanjari na utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Ofisi ilitekeleza yafuatayo:-

Elimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira

56. *Mheshimiwa Spika*, elimu kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira hutolewa katika maadhisho ya Siku ya Mazingira Duniani tarehe 1-5 Juni; maadhisho ya Siku ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa tarehe 17 Juni; na Maadhisho ya Kimataifa ya Tabaka la Ozoni tarehe 15-16 Septemba za kila mwaka kwa kutumia hotuba za viongozi, vipeperushi, mabango, machapisho na vitabu vyenye ujumbe kuhusu masuala ya mazingira. Aidha, Ofisi imeendelea kusambaza nakala za Mpango Kazi wa Taifa wa Mazingira (National Environmental Action Plan - NEAP) wa mwaka 2013-2018 kwa Wizara na Mikoa yote na wadau wengine nchini kwa ajili ya kukuza uelewa wao, kuhusu majukumu waliyonayo katika kuhifadhi na kusimamia mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira.

Ripoti ya Hali ya Mazingira Nchini

57. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Ripoti ya Pili

ya Hali ya Mazingira Nchini ya mwaka 2014, imekamilika, kuchapishwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 22 Aprili, 2015 na Mheshimiwa **Dkt. Mohammed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa ujumla, Ripoti imeonesha kuendelea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira nchini pamoja na juhudzi zinazoendelea kufanywa. Aidha, Ripoti imebainisha kuwepo kwa changamoto mpya za mazingira hususan, taka zinazotokana na vifaa vya umeme na ki-elekroniki, viumbe vamizi vigeni, viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na biofueli, na kubainisha mbinu ya kupambana na hayo. Katika kipindi cha mwaka 2015/16, Ofisi itaendelea kusambaza Ripoti hii na kuelimisha na kuhamasisha umma jinsi ya kukabiliana na changamoto zilizobainishwa. Ripoti hii pia itawasilishwa Bungeni.

Tathmini za Athari kwa Mazingira Kimkakati

58. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na kufanya Tathimini ya Athari kwa Mazingira (TAM), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 imeelekeza pia kufanyika kwa Tathmini ya Mazingira Kimkakati (Strategic Environmental Assessment-SEA) katika uandaaji wa sera, miswada, kanuni, mipango, mikakati au programu mbalimbali kabla ya utekelezaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2014/15 jumla ya mipango kumi na mbili (**12**) ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati ilisajiliwa. Kati ya mipango hiyo, jumla ya Ripoti sita (**6**) za Tathmini ya Mazingira Kimkakati ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji.

59. *Mheshimiwa Spika*, Ripoti za Tathmini zilizoidhinishwa ni: Mpango wa Ukuzaji Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT); Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Mfumo wa Usafirishaji Tanzania (Comprehensive

Transport System Development Master Plan in Tanzania); Mpango wa Uendelezaji wa Eneo la Pwani la Jiji la Dar es Salaam (Waterfront City Development Plan at the Coastal area of Dar es Salaam City); Mpango wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Tengeru, Wilaya ya Meru, mkoani Arusha (Tengeru Satellite Town Development, Meru District, Arusha Region); Mpango wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Themi ya Simba Arusha (Satellite Town Development at Themi ya Simba Arusha District, Arusha Region); na Mpango Kabambe wa Ukanda Maalum wa Uwekezaji Bagamoyo (Bagamoyo Special Economic Zone Master Plan, 2015).

60. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2015/16 Ripoti za Tathmini ya Mazingira Kimkakati kwa ajili ya mipango sita (6) zitaendelea kuandaliwa na kukamilishwa. Mipango iliyopangwa ni:- Mpango wa Uendelezaji wa Mji wa Kisasa katika eneo la Kibada Kigamboni (Kibada Satellite City Development, Temeke District, Dar es Salaam); Mpango wa Uendelezaji Nishati-Kimiminika Tanzania (Liquid Bio-energy Development in Tanzania); Mpango wa Uendelezaji na Mapitio ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Mikoa ya Mtwara na Ruvuma (Development and Review of the Current strategic development plans for Mtwara na Ruvuma Regions); Tathmini ya Usimamizi, Uchimbaji na Uendelezaji wa Mradi wa Maji ya Ardhini katika eneo la Kimbiji (Comprehensive Ground Water Assessment, Supervision of drilling works, development of aquifer monitoring system and evaluation of environmental impact for the Kimbiji aquifer); Mpango Kabambe wa Mafuta na Gesi (Oil and Gas Master Plan); na Mpango Kabambe wa Mfumo wa Usambazaji wa Nishati Tanzania (Power system Master Plan in Tanzania).

61. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki, Ofisi inakamilisha Mwongozo wa

uandaaji wa Tathmini ya Mazingira Kimkakati ambao utatumwiwa na sekta na taasisi za Serikali katika kufanya tathmini hizo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kuzikumbusha wizara na taasisi za Serikali kuzingatia maelekezo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kwa kuandaa ripoti za Tathmini za Mazingira Kimkakati sanjari na maandalizi ya sera, miswada, kanuni, mipango, mikakati au programu katika wizara au taasisi husika.

Hifadhi ya Mazingira katika Maeneo Maalum

62. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2014/15, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilifuatilia na kufanya tathmini ya hali ya mazingira katika Wilaya tatu (3) za Kilolo, Mufindi na Kilombero ambazo zimo ndani ya eneo la lindimaji la Kihansi. Aidha, Baraza liliratibu Programu ya Binadamu na Mazingira Hai (Man and Biosphere Reserve), na linaendelea na mchakato wa kuingiza hifadhi za Jozani, Chwaka Bay na Saadani katika mtandao wa Hifadhi hai wa dunia (World Network of Biosphere Reserves). Mafanikio mengine katika kipindi hiki ni: - Kukamilika kwa Taarifa ya hali ya Mazingira katika Mifumo Ikolojia ya Bwawa la Mtera; kukamilika kwa Taarifa ya hali ya Milima ya Kanda ya Magharibi na Nyanda za juu kusini; na kukusanya taarifa zitakazosaidia kuandaa Taarifa ya Pwani.

Udhibiti wa Mifuko ya Plastiki

63. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kwamba uchafuzi wa mazingira kutokana na mifuko ya plastiki unadhibitiwa, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Rasimu ya kanuni mpya ya mifuko ya plastiki inayoongeza unene wa mifuko kutoka maikroni **30** na kufikia maikroni **50**. Mifuko yenye unene chini ya mikroni **50** haitaruhusiwa kuzalishwa, kuingizwa nchini wala kutumika. Chini ya Kanuni hii baadhi ya bidhaa za plastiki (Polyethelyne materials) zitaendelea kutumika kwa ajili ya

shughuli muhimu viwandani; kama vile viwanda vyatya maziwa, na usindikaji wa vyakula. Aidha, Ofisi imewasiliana na Umoja wa Watengenezaji wa Mifuko ya Plastiki - (Plastic Manufacturers Association of Tanzania – PMAT) kuhusu uwekezaji katika eneo la urejelezaji mifuko ya plastiki. Katika mwaka 2015/16 Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira litaendelea kusimamia kanuni inayoruhusu matumizi ya mifuko ya plastiki yenye unene kiasi cha maikroni **30** na kusisitiza wafanya biashara kutokugawa mifuko hiyo bure. Vile vile, Ofisi itaendelea kuelimisha wadau juu ya umuhimu wa udhibiti wa taka za mifuko ya plastiki na kuhimiza matumizi ya mifuko mbadala.

Vituo vya Huduma Kwa Wasafiri na Wasafirishaji

64. *Mheshimiwa Spika*, ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika barabara kuu nchini, katika kipindi cha mwaka 2015/16 , Ofisi kwa kushirikiana na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali itaandaa utaratibu wa ujenzi wa vituo vya huduma kwa wasafiri na wasafirishaji wanaotumia barabara kuu nchini. Vituo hivyo vitasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira na kuongeza usalama kwa kuepusha ajali zinazosababishwa na uchovu wa madereva. Ofisi kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha sekta binafsi na jamii kwa ujumla kuwekeza katika ujenzi wa vituo hivi muhimu. Vituo hivi vitaanza kujengwa katika barabara za Dar es Salaam hadi Tunduma; Dar es salaam hadi Mwanza; na Dar es salaam hadi Mtwara.

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

65. *Mheshimiwa Spika*, maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yameendelea nchini, Ofisi imewasiliana na Mikoa yote Tanzania Bara kuwakumbusha kuanza maandalizi hayo katika maeneo yao. Maadhimisho hayo hufanyika tarehe **05 Juni** ya kila mwaka. Kwa mwaka

huu 2015, maadhimisho hayo yatafanyika Mkoani Tanga. Kaulimbiu ya mwaka huu ni **Ndoto Bilioni Saba. Dunia Moja. Tumia Rasilimali kwa Uangalifu.** (**Seven Billion Dreams. One Planet. Consume with Care**).

Mfuko wa Taifa wa Manzingira

66. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2014/15, jitihada za kuhakikisha Mfuko wa Taifa wa Mazingira unaanza kufanya kazi zimeendelea. Majadiliano na wadau kuhusu maeneo ya kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya Mfuko yanaendelea. Aidha, Hadidu za rejea za Mtaalam Mwelekezi na Kikosi Kazi cha Kisekta kubaini vyanzo vya fedha vya Mfuko zimeandaliwa. Pamoja na hatua hiyo, Ofisi imefungua Akaunti ya Mfuko na kufanya mawasiliano na Washirika wa Maendeleo, juu ya uanzishwaji wa Mfuko huo, ili waweze kuchangia.

Mfuko wa Mazingira wa Dunia (Global Environment Facility-GEF)

67. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Miradi midogo inayofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP). Chini ya Mfuko huu, miradi midogo saba (7) ya jamii, yenye thamani ya Dola za Marekani **480,507** inatekelezwa. Miradi hiyo inalenga: kuimarisha uwezo wa jamii katika kuhimili mabadiliko ya Tabianchi; kuhifadhi ardhi; kukuza matumizi endelevu ya maliasili; kupunguza umaskini; na kuhifadhi bioanuai na mazingira kwa ujumla. Miradi inatekelezwa katika maeneo ya Wilaya ya Kusini (Makunduchi) Zanzibar na katika mikoa ya Iringa (Pawaga, Kalenga na Isimani), Arusha (Longido), Pwani (Rufiji), Mwanza (Magu) na Morogoro (Uluguru). **Kiambatisho Na.3** cha Kitabu hiki ni Miradi midogo ya hapa nchini inayo fadhiliwa na GEF.

68. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2014 - 2018, Serikali imetengewa jumla ya Dola za Marekani milioni **29.09** kutoka Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Kikao cha wadau cha kupitia maandiko ya miradi na kugawa fedha hizo kilifanyika mwezi Machi, 2015, ambapo zaidi ya miradi **26** ilichambuliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Kitaifa ya Uendeshaji ya GEF kwa ajili ya maamuzi. Kati ya miradi hiyo, jumla ya miradi tisa (**9**) inayohusu Hifadhi ya Bioanuai, Mabadiliko ya Tabianchi, na Usimamizi Endelevu wa Ardhi imepitishwa na kuwasilishwa katika Sekretariati ya Mfuko wa Mazingira wa Dunia kwa hatua zaidi. **Kiambatisho Na.4** ni Miradi iliyopitishwa kufadhiliwa na GEF. Katika mwaka 2015/16, Ofisi itaendelea kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi inayoendelea kutekelezwa chini ya ufadhilli wa mfuko huu. Aidha, Ofisi itaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka katika Mfuko wa Mazingira wa Dunia.

Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira

Mikataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba huu kwa kufanya yafuatayo: Kushirikiana na wadau kuandaa Ripoti ya Tano ya Mikataba na kuiwasilisha Sekretarieti ya Mikataba; Kuratibu mapitio ya Mpango Mkakati wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai kulingana na Mpango Mpya wa Kimataifa wa mwaka 2011 hadi 2020; Kushiriki, kuandaa na kusambaza kwa wadau taarifa ya maamuzi ya Mkutano wa **12** wa nchi wanachama wa Mikataba wa Bioanuai; na kuendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Itifikasi ya Nagoya inayohusu Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Faida Zitokanazo na Matumizi ya Rasilimali za Kijenetiki (The Nagoya Protocol on Access and Benefit Sharing of Genetic

Resources). Vilevile, Ofisi itaendelea kuratibu uridhiaji wa Itifaki ya Ziada ya Nagoya Kuala-Lumpur, inayohusu Uwajibikaji Kisheria Dhidi ya Athari zitokanazo na Matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa (Nagoya-Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety).

Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi

70. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imeendelea kukamilisha taratibu za kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Nairobi, na Itifaki ya Udhhibit wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Aidha, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya na Mamlaka za Mabonde kwa kuhimiza utekelezaji wake. Kazi hii itaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/16.

Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na Itifaki ya Kyoto

71. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2014/15 Ofisi imeendelea kutekeleza shughuli za mabadiliko ya tabianchi. Moja ya majukumu muhimu ni kushiriki kikamilifu katika majadiliano ili kupata Mkataba mpya wa mabadiliko ya tabianchi ambao unatarajiwu kupitishwa mjini Paris mwezi Desemba, 2015. Madhumuni ya Mkataba huu ni kushirikisha nchi zote duniani kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo hazisababishi joto la dunia kuongezeka kwa zaidi ya nyuzijoto mbili (2°C) juu ya kiwango cha sasa, ili kuepuka madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwa binadamu na viumbwe wengine. Aidha, Mkataba utatoa fursa kwa nchi ambazo tayari zinaathiriwa na mabadiliko ya

tabianchi kupewe fedha, teknolojia na kujengewa uwezo wa kuhimili mabidiliko ya tabianchi katika nyanja zote.

72. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Desemba mwaka 2014, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano wa ishirini wa nchi wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi huko Lima, Peru. Maamuzi muhimu ya Mkutano huu ni makubaliano ya kila nchi kuandaa na kuwasilisha maeneo maalumu yatakayokuwa ni mchango wa nchi husika katika juhudzi za dunia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (Intended Nationally Determined Contributions – INDCs). Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na wadau, inafanya mchanganuo wa maeneo muhimu yatakayokuwa ni mchango wa Tanzania katika juhudzi za dunia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hii ya kuandaa INDCs inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu, na kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Mkataba.

73. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi imekuwa na jukumu la kumsaidia Mheshimiwa Rais, akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi za Afrika ya Mabadiliko ya Tabianchi (Commitee of African Heads of State and Government on Climate Change – CAHOSCC). Ofisi imendaa na kuratibu Mikutano minne (4) ya Kamati hiyo ambayo imefanyika chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais, ikiwa ni pamoja na Mkutano Maalumu wa viongozi wakuu wa nchi duniani, kuhusu mabadiliko ya tabianchi ulioitishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwezi Septemba, 2014. Katika kipindi cha uenyekiti wa CAHOSCC Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira alikuwa Katibu wa Kamati hiyo.

74. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania imekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri

wa Mazingira wa Nchi za Afrika (The African Ministerial Conference on Environment – AMCEN) tangu Septemba, 2012 na jukumu hili limeekoma Machi, 2015. Katika kipindi hiki Tanzania kupitia Waziri wa Nchi, wa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira imesimamia majukumu ya kutoa miongozo ya usimamizi wa Mazingira katika Bara la Afrika, na kuhakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya binadamu yanapatikana na yanakuwa endelevu. Katika kutekeleza majukumu haya, AMCEN imeendelea kutoa miongozo kuhusu masuala ya Mazingira ikiwemo utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Hifadhi ya Mazingira.

- 75. *Mheshimiwa Spika*** Ofisi imeratibu maandalizi ya Programu maalum ya Bara la Afrika ya Mabadiliko ya tabianchi, (High Level Work Programme on Climate Change Action in Africa – WPCCAA) chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais. Programu hii imepitishwa na Mkutano wa Umoja wa Afrika mwezi Januari, 2015 na itakuwa dira ya kuongoza nchi za Afrika katika kushughulikia changamoto za mabadiliko ya tabianchi.
- 76. *Mheshimiwa Spika*,** kazi ya kuhuisha masuala ya mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango ya maendeleo ya Serikali imeendelea kutekelezwa. Katika mwaka 2014/15, mafanikio ya miradi ya mabadiliko ya tabianchi iliyotekelizwa Zanzibar na kwenye Wilaya za Igunga, Misenyi, Mbinga, yameandikwa na kusambazwa nchini kwa nia ya kueneza elimu iliyopatikana katika maeneo mengine, ili kuhamasisha wananchi walioathirika na mabadiliko ya tabianchi, kuandaa na kutekeleza miradi kama hiyo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Vile vile, Mradi umeendesha mafunzo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa Maafisa **18**, Madiwani **16**, na viongozi wa vijiji **80** wa halmashauri hizo.

- 77. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2014/15, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii za Pwani ya Bahari ya Hindi Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari. Mradi huu unaotekelawa katika Wilaya za Bagamoyo, Rufiji, Pangani; na Zanzibar. Katika kipindi hiki, Ofisi imetoa mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa maafisa **80** kutoka wilaya hizo na Zanzibar. Aidha, kupitia mradi huu Ofisi imeweka wasimamizi wa Mradi katika maeneo unakotekelawa na kuwapatia usafiri na vitendea kazi.
- 78. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imefikia makubaliano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Huduma za Miradi (United Nations Office for Project Services – UNOPS) ya kufanya upembuzi yakinifu na kuajiri Mkandarasi wa kujenga kuta za bahari za Pangani - Tanga, Kisiwa Panza - Pemba na Kilimani – Unguja. Aidha, katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam, hatua za awali kuhusu maandalizi ya ujenzi wa ukuta wa bahari zitaanza mwaka huu katika maeneo ya Ocean Road na Kigamboni (Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Dar es Salaam), sehemu zilizoharibika kutokana na kuongezeka kwa kina cha bahari, na ukarabati wa baadhi ya miundombinu ya majitaka katika manispaa za Jiji la Dar es Salaam.
- 79. *Mheshimiwa Spika*,** ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, Ofisi imeendelea kutoa mafunzo kwa vikundi vya jamii ya wavuvi na maafisa wa Halmashauri za Manispaa za Temeke, Kinondoni, Ilala na Jiji la Dar es Salaam, juu ya teknolojia za nishati mbadala, na utunzaji wa mazingira ya pwani dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Mpango Kazi wa Kuhuisha masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi katika eneo la Pwani ya Dar es Salaam unaandaliwa.

- 80. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/16, kazi zifuatazo zitatekelezwa katika miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi: kuendelea kuchimba visima vipyta 17 na kujenga mifumo sita (6) ya uvunaji wa maji ya mvua Bagamoyo; kupanda mikoko katika Wilaya za Rufiji na Kinondoni, ili kuzuia mmomonyoko wa fukwe za bahari; na kuanza ujenzi wa kuta za bahari za Pangani na Dar es Salaam. Aidha, maeneo mengine ambako shughuli zitatekelezwa ni pamoja na Kisiwa Panza, Mnazi Mmoja na Kilimani –Zanzibar.
- 81. *Mheshimiwa Spika***, chini ya Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi Ofisi kwa kushikiana na Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika zimeandaa mikakati na mipango ya kisekta ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi (National Adaptation Plans-NAP). Ofisi pia, inatekeleza mpango wa kujenga uwezo katika juhudhi za upunguzaji wa gesijoto kwa kuzingatia maeneo ambayo yataleta maendeleo endelevu, hasa kupitia upatikanaji wa teknolojia na fedha kutoka katika mifuko ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi, kama vile *Green Climate Fund* na mashirika ya kimataifa. Mpango huu ambao unafadhiliwa na UNDP unasadia pia kuweka misingi imara ya kuwa na uwezo wa kuandaa mipango ya kupunguza gesi joto zinazosababisha mabadiliko ya tabianchi, bila kuathiri maendeleo ya nchi (Nationally Appropriate Mitigation Actions -NAMAs).

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame

- 82. *Mheshimiwa Spika***, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Usimamizi Endelevu wa Ardhi Nchini. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imepitia Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame, ili uendane na

Mkakati wa Miaka **10** (2008 - 2018) wa utekelezaji wa Mkataba. Aidha, Taarifa ya hali ya uharibifu wa Ardhi nchini imeandaliwa na kuelekeza mbinu bora za kunusuru maeneo yaliyoharibiwa. Miongozo ya kuhuisha Programu ya Taifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame katika Sera na Mipango ya kisekta imeandaliwa; Vile vile, Ripoti ya Tano ya utekelezaji wa Mkataba na Kitabu cha Mbinu Bora za Usimamizi Endelevu wa Ardhi vimeandaliwa.

- 83. *Mheshimiwa Spika*,** Ofisi inaendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi miwili ya kupunguza uharibifu wa mazingira ya ardhi katika miinuko ya milima mkoani Kilimanjaro (Reducing Land Degradation on the Highlands of Kilimanjaro Regions). Shughuli zilizo fanyika ni: kutoa mafunzo kwa wadau **900** katika masuala ya kisheria, kibiashara na matumizi endelevu ya kuni na mkaa; Ujenzi wa matangi **10** ya maji; na uchimbaji wa mifereji tisa (**9**) na makinga maji. Mradi mwengine ni wa kuhuisha masuala ya usimamizi endelevu wa misitu ya miombo katika Mikoa ya Tabora na Katavi. Wananchi wamewezeshwa kuwa na shughuli mbadala za kuongeza kipato kama ufugaji wa kuku wa kienyeji, ufugaji nyuki, kusindika matunda pori. Vile vile, Mradi umefadhili kikundi cha Akiba na Mikopo – Mbola Uyui ili kuwasaidia wananchi kuweka akiba na kupata mikopo. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa vikundi vyaa ufugaji nyuki na mizinga ya kisasa **310**.
- 84. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za kupambana na kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame, na kutekeleza miradi chini ya Mkataba huu.

Mkataba wa Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni Angani

85. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya kitaifa ya kuondokana na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la hewa ya Ozoni angani. Katika kutekeleza Programu hiyo, mafanikio yaliyopatikana ni:- Mapitio ya mpango wa kuondokana na matumizi ya kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni, inayofadhiliwa na UNDP na UNIDO; na kusambaza jumla ya vifaa **389** vya kuhudumia majokofu, viyoyozi na mitambo ya kupoozea viwandani katika Chuo cha Ufundı cha Arusha; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam; VETA-Kigoma; VETA-Moshi; VETA Kihonda-Morogoro; VETA-Chang'ombe; VETA-Mgulani (JKT); VETA YMCA - Dar es Salaam; Taasisi ya Teknolojia Karume; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; Chuo cha Uvuvi Nyegezi - Mwanza; Chuo cha Uvuvi Mbegani-Bagamoyo; Chuo cha Taifa cha Usafirishaji; na Chuo cha Mafunzo ya Ubaharia - Dar es Salaam.

86. *Mheshimiwa Spika*, warsha ya mafunzo iliyoshirikisha Mafundi **50** wa Majokofu, Viyoyozi na Mitambo ya kupozea viwanda, kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo ilifanyika Jijini Arusha. Washiriki walitoka Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Morogoro na Singida. Aidha, takwimu za mwaka za ungizaji na matumizi ya kemikali na bidhaa zenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni angani zilikusanywa na taarifa kuwasilishwa Sekretariati ya Mkataba. Takwimu hizo zinaonesha kupungua kwa matumizi ya kemikali nchini kwa asilimia **85.7** ukilinganisha na mwaka 1996.

87. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 16 Septemba, 2014, Tanzania iliungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Ozoni. Maadhimisho haya yalifanyika mjini Dodoma ambapo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi

ya Makamu wa Rais -Mazingira alitoa Tamko kwa wanahabari kutoka vyombo vyatuhusu nchini kuhusu umuhimu wa Tabaka la Ozoni kwa afya na mazingira.

88. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2015/16, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mkataba huu nchini kwa kutekeleza kazi zifuatazo:- kukuza uelewa wa jamii kuhusu utekelezaji wa Mkataba na udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni; Kuendesha mafunzo ya wadau juu ya utekelezaji wa sheria na kanuni za kusimamia kemikali hizo; kutekeleza Mpango wa kitaifa wa kupunguza/kusitisha matumizi ya kemikali aina ya *Hydrochlorofluorocarbons - HCFCs* kwa kufuata ratiba iliyowekwa na Mkataba; kukusanya takwimu za uingizaji na matumizi ya kemikali hizo nchini na kuwasilisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa Mkataba kwenye Sekretarieti ya Mkataba.

Mkataba wa Stockholm wa Kudhibiti Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu (Persistent Organic Pollutants)

89. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2014/15, mapitio ya Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm yalifanyika, ili kubainisha hali ya kemikali hizo nchini na hatua zinazochukuliwa kudhibiti athari zake. Kazi hii ilihuisha kukusanya takwimu za kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba huu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Shinyanga na Mwanza. Vile vile, ukaguzi ulifanyika katika maeneo yaliyoharibiwa na kemikali hizi katika mikoa ya Arusha na Morogoro. Aidha, mafunzo ya kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi bora wa kemikali hizi, yalifanyika jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalishirikisha wataalamu **55** kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya

Kilimo, Misitu na Maliasili – Zanzibar; Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO); Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Zanzibar; Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali; Shirika la Usambazaji wa Umeme Tanzania bara (TANESCO); Chuo Kikuu cha Ardhi; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Ofisi ya Makamu wa Rais. Utafiti umebainisha kuwa kemikali mpya zilizoongezwa kwenye Mkataba zipo nchini.

- 90. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kwa kushirikiana na UNEP imeanzisha mtandao wa kupeana taarifa unaojumuisha wadau wote wanaosimamia Kemikali nchini. Mtandao huo unajulikana kama *Chemicals Information Exchange Network - CIEN*. Wataalam **25** kutoka Wizara, Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali walipatiwa mafunzo ya kukusanya na kupeana taarifa zinazohusu kemikali, kupitia mtandao huu. Mtandao huu unalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa kutumia tovuti yenye anwani www.estis.net/sites/cien-tanza. Tovuti hii ina taarifa zinazohusu sera, sheria, mikakati na Miongozo kutoka taasisi zinazohusika na usimamizi endelevu wa matumizi ya kemikali nchini.
- 91. *Mheshimiwa Spika*,** kwa mwaka 2015/16, Ofisi itakamilisha mapitio ya Mpango wa Taifa wa utekelezaji wa Mkataba; na itatoa elimu na kukuza uelewa kwa wadau kuhusu madhara kwa afya na mazingira yanayosababishwa na kemikali za awali na zile mpya zinazodhibitiwa na Mkataba. Aidha, itahamasisha matumizi ya kemikali mbadala zilizopo; itachapisha na kusambaza nakala za Mpango huo kwa wadau; na kuandaa ripoti ya utekelezaji wa Mkataba huu, na kuiwasilisha Sekretarieti ya Mkataba.

Mkataba wa Basel kuhusu Udhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu Bainya ya Nchi na Nchi na Mkataba wa Bamako unaozuia Uingizaji wa Taka za Sumu Barani Afrika

92. *Mheshimiwa Spika*, kuitia mkataba huu, Ofisi imefanya utafiti kuhusu usimamizi endelevu wa matairi chakavu na yaliyokwisha muda wa kutumika. Utafiti huu ulifanyika ili kubainisha changamoto na hatua za kudhibiti taka hizo; Warsha ya kubadilishana uzoefu katika usimamizi wa taka za matairi ilifanyika Dar es Salaam na wadau **30** walishiriki Ufutiliaji na ukaguzi wa tani **3000** za taka hatarishi za betri chakavu za magari ulifanyika, na kibali kutolewa kwa kampuni ya TANKO ya Dar es Salaam, kusafirisha taka hizo kwenda nchini Korea kwa ajili ya urejelezaji. Aidha, ufuutiliaji na ukaguzi wa tani **200** za taka hatarishi za vifaa vya umeme na elektroniki ulifanyika na kibali kilitolewa kwa Kampuni ya OK Plastic Ltd, ya Dar es Salaam kusafirisha taka hizo kwenda Ubelligiji kwa ajili ya urejelezaji.

93. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2015/16, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba iliyotajwa.

MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2005 HADI 2015

94. *Mheshimiwa Spika*, katika kusimamia hifadhi ya mazingira nchini, mafanikio yafuatayo yamepatikana katika kipindi hiki katika kusimamia utekelezaji Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 :-

Kanuni 25 na Miongozo 10 vimeandaliwa. Aidha, Miongozo iliyoandaliwa inatumika katika kuandaa Mipango Kazi ya Mazingira katika ngazi ya Wizara na Serikali za Mitaa ili kupunguza uharibifu wa mazingira nchini. Mafanikio mengine ni kutolewa kwa Ripoti mbili (2) za Hali ya Mazingira nchini ambapo Ripoti ya kwanza ilitolewa mwaka 2008 na ya pili mwaka

2014. Ripoti hizi zimeonesha kuendelea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira nchini, pamoja na juhudini zinazoendelea kufanyika. Aidha, Ripoti ya mwaka 2014 imebainisha kuwepo kwa changamoto mpya za mazingira. Ripoti hizi ni muhimu katika kuandaa mipango ya maendeleo.

95. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira imeendelea kusimamia na kuhakikisha kwamba Miradi ya maendeleo inafanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Miradi ilifanyiwa Tathmini za Athari kwa Mazingira na vyeti vya TAM **1,846** vilitolewa. Hatua hizi zimesaidia kupunguza athari kwa mazingira na hivyo kuchangia maendeleo endelevu.

96. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya viwanda **935**, migodi mikubwa na ya kati **121**, vituo vya mafuta **161**, mahoteli ya kitalii **74**, mashamba makubwa matatu (3) yalifanyiwa ukaguzi, na hatua za kisheria kuchukuliwa, ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

97. *Mheshimiwa Spika*, katika kuoanisha maendeleo endelevu na kupunguza umaskini, Baraza liliandaa Agenda ya Kitaifa ya Utafiti wa Mazingira. Vilevile, tathmini ya hali ya milima imeandaliwa kwa Kanda za Kusini, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini. Taarifa hizi zimesaidia kuainisha maeneo ambayo yanahitaji uhifadhi maalumu. Elimu ya hifadhi ya mazingira kwa umma imetolewa kupitia maadhisho na maonesho ya Siku ya Mazingira Afrika; Siku ya Mazingira Duniani; Siku ya Utumishi wa Umma; Siku ya Wakulima Nanenane na Siku ya Ozoni Duniani. Aidha, elimu ilitolewa pia kwa kutumia njia zifuatazo: vipeperushi, mabango na vitini; magari ya matangazo, televisheni, redio na makala kwenye magazeti; na maonesho ya matumizi ya majiko banifu. Vilevile, elimu kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira na TAM imetolewa kwa Maafisa Mazingira wa

Serikali za Mitaa katika Mikoa yote ya Tanzania bara. Elimu inayoendelea kutolewa imechangia katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na kuongeza uelewa wa jamii na hivyo kupunguza uharibifu wa Mazingira.

98. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imepitisha mikakati miwili (2) kwa lengo la kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji, mazingira ya ardhi na misitu. Mikakati hiyo ni: Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006; na Mkakati wa Hatua za Haraka za kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008. Hatua hizi zimesaidia kuimarisha hifadhi ya mabonde na vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Tuzo ya Rais ya Kuhifadhi Vyanzo vya Maji, Kupanda na Kutunza Miti imetolewa mara tatu. Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti inayozitaka kila Halmashauri nchini kupanda miti **1,500,000** kila mwaka imeendelea kutekelezwa. Kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2015 Ofisi ya Makamu wa Rais ilipokea taarifa za upandaji miti kutoka mikoani, zinazoonesha kuwa miti **1,491,870,192** ilipandwa na kati ya hiyo miti **1,139,473,928** imestawi, sawa na asilimia **76.2**.

99. *Mheshimiwa Spika*, uratibu wa utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira imewezesha kuandaliwa kwa Mpango na Programu ifuatayo:- Mpango kazi wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2013-2018); Mpango wa Taifa wa Kusimamia Kemikali Zinazodumu kwa Muda Mrefu katika Mazingira wa mwaka 2007; Programu ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi ya Mwaka 2007; Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame; na Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa Unaotokana na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu. Aidha, Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mkakati wa Mawasiliano wa Kuhimili

Mabadiliko ya Tabianchi imeandaliwa na inaendelea kutekelezwa.

100. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira, changamoto zifuatazo zimejitokeza:- Sekta, Serikali za Mitaa na wadau wengine walioainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kutotekeleza matakwa ya Sheria kwa ukamilifu wakidhani kuwa, utekelezaji wa Sheria hii ni jukumu la Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza pekee; Sekta na Serikali za Mitaa kutohuisha na kutekeleza kikamilifu masuala ya mazingira katika Mipango na bajeti zao; Ufinyu wa bajeti unaosababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya shughuli zilizopangwa, katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa; Uhaba wa watumishi na vitendea kazi katika kusimamia masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira katika sekta zote; Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira; Athari za mabadiliko ya Tabianchi; Kukosekana kwa takwimu sahihi za mazingira na kwa wakati; na hali ya umaskini katika jamii.

IV. MASUALA YA UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

101. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2014/15, Ofisi imeendelea kuwawezesha watumishi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi hiki, watumishi **66 waliwezeshwu kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi, yanayohusiana na taaluma zao, ili kuongeza ujuzi mbalimbali na uwezo katika utendaji wa kazi. Aidha, Ofisi imejaza nafasi za ajira mpya **15**; kuwapandisha vyeo watumishi **29**; na kuwabdalisha kada watumishi wawili (**2**) wenye sifa. Taarifa za watumishi wa Ofisi zimehakikiwa na kuboreshwa kwa kutumia mfumo wa taarifa za watumishi na mishahara (Human Capital Management Information System).**

102. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki maslahi, stahili na haki za watumishi zimeendelea kutolewa kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na Miongozo iliyotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi imeendelea kutekeleza Mfumo wa Wazi wa mapitio na tathmini ya utendaji kazi wa watumishi (Open Performance Review Appraisal System - OPRAS).

103. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa 2014/15 Ofisi imeendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kufanikisha upatikanaji wa vitendea kazi kwa kuzingatia uwezo kifedha. Aidha, ukamilishwaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais, Awamu ya Pili, lililopo Mtaa wa Luthuli, Dar es Salaam pamoja na Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Tunguu Zanzibar umesimamiwa kikamilifu. Aidha, Mradi wa Jengo la Ofisi za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, eneo la Regent Estate, Dar es Salaam unaendelea kukamilisha maandalizi ya michoro ya ujenzi, na pia kukamilisha mazungumzo ya kujenga jengo hilo kwa kushirikiana na mbia.

104. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Ofisi iliendelea kuzingatia misingi ya utawala bora, demokrasia na ushirikishwaji wa watumishi mahala pa kazi katika kupanga na kutekeleza majukumu ya Ofisi, kupitia vikao viwili (2) vya Baraza la Wafanyakazi pamoja na vikao vya Idara na Vitengo.

105. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki Ofisi imeimarisha mahusiano, ushirikiano na mshikamano kwa watumishi wake na watumishi wa Ofisi nyingine za Serikali kupitia michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Morogoro na SHIMUTA iliyofanyika Tanga. Aidha, watumishi wameshiriki kikamilifu

katika mazoezi ya viungo, ili kuimarisha afya zao na kuwajengea ukakamavu na hatimaye kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

106. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu iliyoko kabidhiwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo iliyowekwa katika Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi itaendelea kutathmini utendaji kazi wa watumishi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi kwa watumishi (Open Performance Review and Appraisal System – OPRAS). Aidha, kumbukumbu za watumishi zitaendelea kuboreshwa kwa kutumia Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Mishahara (Human Capital Management Information System), pamoja na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza shughuli zilizopangwa.

107. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2015/16 Ofisi itaendelea kuratibu utoaji wa elimu ya UKIMWI kwa watumishi wake na kuwashawishi kupima afya zao kwa hiyari, kuwapatia ushauri nasaha na utoaji huduma kwa watumishi watakaobainika kuwa na maambukizi. Aidha, Ofisi itendelea kuwapatia watumishi stahili, maslahi na haki zao ikiwa ni pamoja na kuwapandisha vyeo na kuwathibitisha kazini, kwa kuzingatia sifa na miundo inayotawala kada zao, na kuwapatia vitendea kazi. Nafasi mpya za ajira thelathini na moja (31) zinatarajiwa kujazwa kwa kuzingatia Ikama itakayoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

108. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2015/16 Ofisi itasimamia ukarabati wa jengo kuu la Ofisi lililopo Mtaa wa Luthuli na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais yaliyopo Oysterbay – Dar es Salaam, Kilimani Dodoma na Wete Pemba. Aidha, Ofisi za Baraza zitafanyiwa ukarabati mdogo ili kuboresha mazingira ya kazi katika majengo yaliyopo.

VI. SHUKRANI NA HITIMISHO

109. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutoa shukrani zangu kwa Mawaziri wenzangu, Mheshimiwa Mhandisi **Dkt. Binilith Satano Mahenge (Mb.)**, Waziri wa Nchi mwenye dhamana ya Mazingira, na Mheshimiwa **Stephen Julius Masele (Mb.)**, Naibu Waziri – Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano na utendaji wao thabiti na makini, katika kutekeleza majukumu ya Ofisi.
110. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Watendaji Wakuu katika Ofisi ya Makamu wa Rais, **Bw. Sazi Bundara Salula - Katibu Mkuu**, Mhandisi **Angelina Elias Madete** – Naibu Katibu Mkuu, na Mhandisi **Bonaventure Thobias Baya** - Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Nawashukuru na kuwapongeza pia Wakuu wa Idara na Vitengo, na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa juhudzi zaao za dhati, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Vile vile, napenda kuwashukuru wale wote walioituwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na kufanikisha kuandaa mipango ya mwaka wa fedha 2015/16 na hivyo kustawisha hoja ambayo nimeiwasilisha hapa leo.
111. *Mheshimiwa Spika*, naomba pia nitumie fursa hii ya kipekee, kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi, kwa mwaka wa fedha 2014/15. Baadhi ya nchi na Mashirika ya Kimataifa yafuatayo yameshiriki katika kusaidia ufanikishaji wa shughuli zilizolengwa:- Serikali ya Marekani; Serikali ya Norway; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Mfuko wa Mazingira wa

Dunia (GEF); Benki ya Dunia (IDA); Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA); Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA); *World Wildlife Fund* (WWF); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); *International Institute of Tropical Agriculture* – (IITA); Taasisi ya Kimataifa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); na Sekta Binafsi. Napenda kuwaomba washirika wa maendeleo kuendelea kushirikiana nasi mwaka wa fedha 2015/16 katika kufikia malengo yaliyowekwa ya kuhifadhi Mazingira na kudumisha Muungano wetu.

VII. MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/16

112. *Mheshimiwa Spika*, ili Ofisi ya Makamu wa Rais, iweze kutekeleza ipasavyo malengo yaliyoelezwa katika Hotuba hii, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2015/16 kama ifuatavyo:

FUNGU 26: MAKAMU WA RAIS

113. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **5,079,085,000/=** fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ajili ya Fungu hilo. Kiasi hicho kinajumuisha fedha za Mishahara shilingi **1,480,676,000/=** na fedha za Matumizi Mengineyo shilingi **3,598,409,000/=**

FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS

114. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi inaombwa kuidhinishiwa jumla ya shilingi **38,077,215,000/=** zikijumuisha fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi **33,558,368,000/=** na fedha za Maendeleo shilingi **4,518,847,000/=**. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi **3,200,337,000/=** Mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais; na shilingi **30,358,031,000 /=** Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Matumizi Mengineyo zinajumuisha

shilingi **22,400,000,000/=** gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; shilingi **3,592,326,000/=** ruzuku kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na kiasi kinachosalia cha shilingi **4,365,705,000/=** ni fedha za Matumizi Mengineyo za Idara na Vitengo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Kwa upande wa fedha za Maendeleo zinajumuisha shilingi **3,500,000,000/=** fedha za ndani; na shilingi **1,018,847,000/=** fedha za nje.

115. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa Hoja.

KIAMBATISHO NA.1

TAARIFA ZA UPANDAJI MITI KITAIFA KWA MWAKA 2013/14

S/N	MKOA/WILAYA	LENGO	UTEKELEZAJI		
		(IDADI)	Idadi ya miti iliyopandwa	Idadi ya miti iliyostawi	Asimilia ya Miti iliyostawi
1	RUVUMA				
	Tunduru	500,000	370,000	285,000	74
	Namtumbo	3,000,000	2,350,000	1,880,000	80
	Songea	3,000,000	4,262,410	3,196,808	75
	Mbinga	3,000,000	3,074,640	2,490,458	81
	Jumla ndogo	12,000,000	12,339,350	9,554,022	77.4
2	MBEYA				
	Chunya	1,500,000	716,300	512,212	72
	Ileje	2,000,000	3,361,585	3,053,421	91
	Kyela	100,000	67,521	63,470	94
	Mbarali	1,000,000	960,100	650,480	68
	Mbeya Jiji	400,000	319,000	223,300	70
	Mbeya Vijijini	1,500,000	898,900	736,852	82
	Mbozi	600,000	328,670	233,356	71
	Rungwe	1,500,000	1,564,311	1,126,303	72
	Busokelo		7,375	7,152	97
	Momba	1,500,000	540,210	421,103	78
3	Jumla ndogo	10,100,000	8,763,972	7,027,649	80.2
	KILIMANJARO				
	Hai		903,325	695,561	77
	Mwanga	1,000,000	710,183	423,857	61
	Rombo	2,500,000	1,945,430	1,698,523,	87
	Moshi (M)	1,600,100	994,723	760,963	77
	Moshi (V)	1,122,808	978,570	632,571	65
	Siha	1,148,130	1,538,329	1,355,136	88
	Same	1,500,000	1,342,600	980,098	73
	Jumla ndogo	10,371,038	8,413,160	6,555,709	72.6
4	IRINGA				
	Iringa	1,500,000	1,583,500	1,350,000	85
	Mufindi	37,531,000	35,133,510	33,545,510	96
	Kilolo	12,000,000	20,922,170	20,145,213	96
	Iringa Manispaa	1,500,000	300,000	272,000	91
5	Jumla ndogo	52,531,000	57,939,180	55,312,723	95.5
	LINDI				
	Nachingwea	1,500,000	353,050	352,951	99
	Liwale	1,500,000	874,524	642,775	74
	Lindi	1,500,000	1,225,000	857,500	70
	Kilwa	1,500,000	1,200,000	968,185	81
	Ruangwa	1,500,000	923,000	780,000	85
	Manispaa ya Lindi	20,000	13,500	12,121	90
	Jumla ndogo	7,520,000	4,589,074	3,613,532	79
6	RUKWA				

	Kalambo	1,500,000	770,337	547,456	71
	Manispaa	1,000,000	834,176	791,448	95
	Nkasi	2,000,000	77,977	65,142	84
	Sumbawanga	1,000,000	595,760	417,032	70
	Jumla ndogo	5,500,000	278,250	1,821,078	80
7	KIGOMA				
	Kasulu	1,500,000	633,403	380,042	60
	Kibondo/Kakonko	1,500,000	800,000	480,000	60
	Kigoma	1,500,000	69,000	41,400	60
	Buhigwe	2,000,000	600,000	360,000	60
	Uvinza		98,000	58,800	60
	Kigoma/Ujiji	1,500,000	342,000	205,200	60
	Jumla ndogo	8,000,000	2,542,403	1,525,442	60
8	KATAVI				
	Mji Mpanda	100,000	42,650	29,002	68
	Nsimbo	750,000	692,000	452,568	65
	Mpanda	750,000	518,128	433,673	84
	Mlele	700,000	615,000	540,339	88
	Jumla ndogo	2,300,000	1,867,778	1,455,582	78
9	MARA				
	Bunda	1,500,000	819,980	524,788	64
	Butiama	1,500,000	916,000	864,812	94
	Musoma DC	750,000	503,840	378,421	75
	Musoma MC	500,000	342,564	307,680	89
	Tarime DC	1,500,000	827,139	661,712	55
	Tarime TC	300,000	100,250	88,088	87
	Serengeti	1,500,000	1,080,000	677,280	72
	Rorya	1,500,000	950,000	832,500	87
	Jumla ndogo	9,050,000	5,539,773	4,335,281	78
10	MWANZA				
	Misungwi	1,500,000	789,569	679,545	86
	Ukerewe	1,500,000	841,000	681,780	81
	Kwimba	1,500,000	832,024	520,214	63
	Sengerema	1,500,000	1,376,494	1,032,371	75
	Mwanza Jiji	1,500,000	2,448,639	2,081,344	85
	Ilemela Manispaa	1,500,000	987,000	952,000	97
	Magu	1,000,000	611,787	395,861	65
	Jumla ndogo	10,000,000	7,787,753	6,343,115	78.8
11	NJOMBE				
	Ludewa	1,500,000	5,306,738	5,196,362	98
	Njombe DC	6,000,000	8,435,466	7,085,792	84
	Njombe TC	5,000,000	15,410,631	14,530,215	94
	Makete	5,000,000	9,341,175	8,647,538	93
	Makambako	1,500,000	2,438,661	2,242,756	92
	Wanging`ombe	1,500,000	2,567,329	2,198,640	86
	Jumla ndogo	20,500,000	43,500,000	39,901,303	92
12	TABORA				
	Uyui	1,500,000	1,847,000	1,622,000	88
	Sikonge	1,500,000	982,800	737,100	75
	Nzega	1,500,000	1,300,690	493,765	38

	Igunga	1,500,000	665,000	500,000	75
	Urambo	2,000,000	1,525,663	1,144,247	75
	Tabora (M)	1,500,000	989,027	758,934	77
	Kiliua	1,500,000	1,437,000	287,400	20
	Jumla ndogo	11,000,000	8,747,180	5,543,446	64
13	MOROGORO				
	Ulanga	1,500,000	858,750	809,166	94
	Gairo	1,500,000	700,000	644,000	92
	Kilombero	1,500,000	2,700,000	2,320,000	86
	Manispaa Morogoro	750,000	700,000	540,000	77
	Kilosa	1,500,000	778,200	544,740	70
	Mvomero	1,500,000	1,100,000	750,000	68
	Morogoro D.C	1,500,000	1,000,000	800,000	80
	Jumla ndogo	9,750,000	7,836,950	6,407,906	82
14	MTWARA				
	Newala	1,500,000	878,349	794,217	90
	Nanyumbu	1,500,000	965,000	797,250	83
	Mtwara (V)	1,500,000	97,430	82,603	85
	Tandahimba	1,500,000	252,789	188,960	75
	Masasi	1,500,000	27,000	18356	68
	Manispaa Mtwara	1,500,000	21,000	15786	75.
	Jumla ndogo	9,000,000	2,241,138	1,897,172	84.7
15	PWANI				
	Rufiji	500,000	221,056	77,370	35
	Kibaha TC	400,000	273,600	131,328	48
	Kibaha DC	500,000	340,650	119,228	35
	Mkuranga	400,000	120,000	54,000	55
	Bagamoyo	1,200,000	785,066	235,520	30
	Mafia	70,000	34,940	24,458	70
	Kisarawe	640,000	508,123	315,036	62
	Jumla ndogo	3,710,000	2,283,435	956,940	42
16	TANGA				
	Lushoto	2,000,000	2,602,140	1,821,498	70
	Kilindi	1,500,000	1,976,000	1,600,000	81
	Pangani	2,000,000	1,500,000	825,000	55
	Mkinga	2,000,000	2,002,042	1,600,200	80
	Handeni	1,500,000	881,210	442,100	50
	Korogwe	1,000,000	1,086,032	868,830	80
	Muheza	2,000,000	2,336,919	1,852,689	79
	Tanga Jiji	3,000,000	3,118,000	1,200,000	39
	Bumbuli	1,500,000	1,268,839	1,015,072	80
	Jumla ndogo	16,500,000	16,771,182	11,225,359	68.2
17	SHINYANGA				
	Ushetu	1,500,000	29,749	23,107	78
	Kahama (M)	1,500,000	22,649	17,250	76
	Msalala	1,500,000	30,490	28,348	93
	Kishapu	1,500,000	246,218	230,872	94
	Shinyanga (V)	1,500,000	171,682	168,572	98
	Shinyanga (M)	1,500,000	983,405	979,340	99
	Jumla ndogo	9,000,000	1,484,193	1,447,489	97.5

18	DODOMA				
	Mpwapwa	1,500,000	563,000	270,240	48
	Kondoa	1,500,000	872,840	480,062	55
	Kongwa	1,500,000	677,325	284,480	42
	Dodoma (M)	1,500,000	847,880	423,940	50
	Chamwino	1,500,000	655,260	275,210	42
	Bahi	1,500,000	640,620	295,780	46
	Jumla ndogo	9,000,000	4,256,925	2,029,712	48
19	SIMIYU				
	Bariadi	2,500,000	903,415	604,133	67
	Maswa	2,500,000	303,481	278,943	92
	Meatu	2,500,000	2,855,776	2,107,765	74
	H/Mji/Bariadi	2,500,000	569,554	300,456	53
	Itilima	2,500,000	304,106	229,908	76
	Busega	2,500,000	208,377	158,654	76
	Jumla ndogo	12,500,000	5,144,709	3,679,859	71.5
20	SINGIDA				
	Ikungi	1,500,000	400,539	150,911	38
	Manyoni	1,500,000	508,492	192,874	38
	Singida	1,500,000	353,478	214,986	61
	Mkalama	1,500,000	98,147	41,345	42
	Iramba	1,500,000	357,000	208,988	59
	Singida Manispaa	1,500,000	1,320,300	534,198	40
	Jumla ndogo	9,000,000	3,037,956	1,343,302	44.2
21	DAR ES SALAAM				
	Ilala	1,500,000	301,100	212,904	71
	Kinondoni	1,500,000	1,100,000	800,500	73
	Temeke	1,500,000	2,085,000	1,287,450	78
	Jumla ndogo	4,500,000	3,486,100	2,297,352	65.9
22	ARUSHA				
	Jiji la Arusha	1,500,000	1,750,000	1,225,000	70
	Monduli	1,500,000	1,500,000	1,308,000	87
	Meru	1,500,000	1,302,070	1,298,715	99
	Halmashauri ya Wilaya Arusha	1,500,000	1,485,650	1,472,157	99
	Halmashauri ya Wilaya Karatu	1,500,000	1,395,528	1,387,238	99
	Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro	1,500,000	700,000	450,000	64
	Halmashauri ya Wilaya longido	1,500,000	317,941	305,766	96
	Jumla ndogo	10,500,000	8,451,189	7,446,876	88
	JUMLA KUU	252,332,038	217,301,650	181,720,849	83.63

KIAMBATISHO NA.2

ORODHA YA WASHINDI WA TUZO KWA MWAKA 2014 PAMOJA NA ZAWADI ZAO

SN	JINA LA MSHINDI	KUNDI LA MSHINDI	WILAYA/MKOA	AINA YA ZAWADI
1	Bw. Leons Nombo	Kaya bora	Mbinga, Ruvuma	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs 2,000,000/=
2	Kijiji chs Nyamayinza	Kijiji bora	Misungwi, Mwanza	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs 3,000,000/=
3	Kata ya Kalebezo	Kata bora	Sengerema, Mwanza	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs

				3,000,000/=
4	Shule ya Msingi Huruma	Shule ya Msingi Bora	Mbinga, Ruvuma	Cheti, Kombe na Pesa Taslimu shs 3,000,000/=
5	Shule ya Sekondari Anderleck Ridges	Shule ya Sekondari Bora	Kahama, Shinyanga	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs 3,000,000/=
6	Chuo cha Utafiti wa Kilimo cha Igabilo	Chuo cha Mafunzo Bora	Muleba, Kagera	Cheti, Kombe na Pesa Taslimu shs 5,000,000/=
7	Taasisi ya Mavuno Village	Taasisi ya Uhamasishaji Bora	Magu, Mwanza	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs 3,000,000/=
8	Kiwanda cha Sukari TPC	Taasisi ya Uwezeshaji Bora	Moshi, Kilimanjaro	Cheti na Kombe
9	Mzinga JWTZ	Taasisi ya Kijeshi Bora	Morogoro Manispaa	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs 5,000,000/=
10	Wilaya ya Kishapu	Wilaya Bora	Kishapu, Sinyanga	Cheti, Kombe na Pesa taslimu shs 5,000,000/=
11	Bw. Leons Melkion Nombo	Mshindi wa Jumla	Mbinga, Ruvuma	Ngao na Pesa taslimu Shs. 10,000,000/=

KIAMBATISHO NA.3

MIRADI MIDOGO ILIYOFADHILIWA CHINI YA GEF (SMALL GRANTS PROGRAMME), 2014

SN	JINA LA MRADI	FEDHA ILIYOOMBWA USD
1.	Supporting Community Based Adaptation Initiatives to cope with adverse effects of Climate Change in three divisions of Pagawa, Kalenga and Isimani in Iringa Rural District	48,766
2.	Enhancing Climate Change resilience strategies to the most vulnerable in Longido District Communities	99,940
3.	Conservation and Sustainable Land Management in Makunduchi, Zanzibar	48,766
4.	Promotion of Sustainable Conservation and Utilization of Natural Resources for Poverty Reduction and Community Development around Rufiji Forest Reserve.	74,654
5.	Promotion of Integrated Aquaculture and Natural Resources Management for Restoring Lake Environmental Health, Poverty Reduction and Household Food Security, Magu, Mwanza	97,532
6.	Children as Catalysts of Environmental Change, Mwanza	9,103

7.	Conservation of Biodiversity – rich Uluguru Mountain Forest through Wider Adoption of Biogas Plants, Morogoro	101,746
	JUMLA	480,507

KIAMBATISHO Na. 4

ORODHA YA MIRADI ILIYOPITISHWA KUFADHILIWA NA GEF MWAKA 2014 - 2018

SN	Project Title	Proponent	Budget USD (000,000)
1.	Integrated Biodiversity Conservation Project	Ministry of Agriculture and Natural Resources -Zanzibar,	3.00
2.	Strengthening Climate Change Mitigation Actions in Zanzibar, United Republic of Tanzania	First Vice President's Office - DOE ZANZIBAR	2.83
3.	Strengthening capacity for implementation of integrated ecosystem management approach for SLM, Biodiversity conservation and climate change resilience in Tanzania	VPO-Division of Environment	5.053
4.	Combating Poaching and illegal wildlife trade in Tanzania through integrated approach	Ministry of Natural Resource and Tourism	6.00
5.	Promotion of bio-ethanol as alternative fuel for cooking	Ministry of Energy and Minerals	2.80
6.	Sustainable Land Management in the Usangu Wetland and its Catchments	National Environment Management Council	2.86
7.	Small Grants Programme Project	UNDP	2.00
8.	Preparation of intended nationally Determined contribution (INDC) to the 2015 agreement under United Framework Convention on Climate Change	Vice President's Office	0.547
9.	Reversing land Degradation Trend and Increasing Food Security in Degraded Ecosystems of Semi-arid of Central Tanzania	Vice President's Office, MAFC, MoW	4.00
TOTAL			29.09